# AckySHINE.com

# Mambo 7 ya kubadili katika maisha ili ubadilike

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · January 17, 2017

Mafundisho ya Msingi ya Kanisa Katoliki: Makala za Katoliki · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Ushauri kuhusu mambo mbalimbali Katika Maisha

1. Huwezi kubadili namna watu walivyokutendea mpaka ubadili namna unavyowatendea.

Matayo 7:12; "Basi yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo Torati na Manabii."

2. Huwezi kubadili tabia mpaka ubadili marafiki.

1Wakorintho 15:33 "Msidanganyike; Mazungumzo mabaya huharibu tabia njema."

3. Huwezi kubadili ulichovuna mpaka ubadili ulichokipanda.

Wagalatia 6:7; "Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna."

4. Huwezi kubadili mwelekeo wa maisha yako mpaka ubadili dereva.

Kutoka 23:1-3; "Msivumishe habari za uongo; usishirikiane na mwovu kwa kuwa shahidi wa uongo. Usiwafuate walio wengi katika kutenda uovu; wala usitie ushahidi wako katika neno lolote kwa kugeukia kando na kuandamana na mkutano ili kupotosha hukumu; wala usimpendelee mtu mnyonge katika neno lake".

Maisha yako yaweza ongozwa na mkumbo wa watu au MSIMAMO wako BINAFSI kwa UNACHOKIAMINI.

5. Huwezi kubadili hali yako ya kifedha mpaka ubadili tabia yako ya kifedha.

Mithali 21:17; Mtu apendaye anasa atakuwa maskini; yeyote apendaye mvinyo, kula na manukato hatakuwa tajiri."

Mtindo wa maisha ya ufukara ndiyo busara kwa wengi.

6. Huwezi kunibadili mpaka ujibadili mwenyewe.

Matayo 7:3-5. "Basi, mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huioni? Au utamwambiaje nduguyo, Niache nikitoe kibanzi katika jicho lako; na kumbe! Mna boriti ndani ya jicho lako mwenyewe? Mnafiki wewe, itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoa kile kibanzi katika jicho la ndugu yako."

7. Huwezi kubadili mtazamo wako wa kifikra mpaka ubadilipo usikiacho.

Mithali 23:7; "Maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo. Akuambia haya kula, kunywa; lakini moyo wake hauwi pamoja nawe."

(Waache wenye Hekima wasikilize na kuongeza ufahamu wao.)

Huyo anayesikiliza, huashiria na kuamua kile anachojifunza.

Kile unachojifunza, huashiria uelewa ulio nao kichwani mwako.

Uelewa ulionao kichwani mwako, huashiria maamuzi yako.

Na maamuzi yako, huashiria mwelekeo wa maisha yako.